

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
Mtaa wa Makole
S.L.P. 941,
41105 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Katibu wa Bunge anautaarifu Umma wa Watanzania kuwa tarehe 31 Januari, 2022 Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb aliyekuwa Naibu wa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alijiuzulu nafasi hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 149(1) (c) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano baada ya kuteuliwa na chama chake cha CCM kuwa Mgombea wa nafasi ya Spika wa Bunge. Hivyo, nafasi ya Naibu wa Spika wa Bunge iko wazi.

Katika mazingira hayo, masharti ya Ibara ya 85(3) (b) na 86(2) ya Katiba, yanaelekeza kufanyika Uchaguzi kujaza nafasi ya Naibu wa Spika wa Bunge mapema iwezekanavyo mara baada ya kiti cha Naibu wa Spika kuwa wazi.

Kila chama cha siasa chenye uwakilishi Bungeni kinayo haki ya kushiriki katika uchaguzi huo kwa mujibu wa Ibara ya 85(1) ya Katiba. Chama kinachokusudia kushiriki Uchaguzi, kinashauriwa kuanza mchakato wa kumpata Mgombea kutoka miongoni mwa Wabunge wa chama hicho.

Uchaguzi umepangwa kufanyika tarehe 11 Februari, 2022. Hivyo, jina la Mgombea linapaswa kuwasilishwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi kabla ya Saa 10:00 Jioni siku ya Alhamisi tarehe 10 Februari, 2022 katika Ofisi ya Katibu wa Bunge iliyopo katika Jengo la Bunge, Barabara ya Dar es Salaam, Mtaa wa Makole, Dodoma.

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
DODOMA.

03 Februari, 2022